ana na
ku-
nchini
mka-
noja
umri
a
kiwa
yenye
ikuwa
ka
ılu.
ye-
a
na
-
na
na
a na

...wa Wilaya ya Butiama, Moses Kaegele akimtambulisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa kwa watendaji na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa wilaya hiyo wakati wa ziara yake ya kikazi ya kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma. (Picha na Ofisi ya Rais).

HABARI LEO UK 20.

# Waziri ataka wafugaji wanunue maeneo ya malisho

**Na Baraka Messa, Songwe**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka wafugaji kuanza kununua maeneo yao ya kufugia mifugo.

Alitoa mwito huo juzi wakati akizungumza na wafugaji wa maeneo ya Kapele, Ikana, Mpapa na Samang'ombe wilayani Momba kwenye ziara yake ya siku mbili.

Alisema hatua hiyo itasaidia kutatua changamoto ya migogoro kati yao na wakulima ambayo huibuka kutokana na mifugo kuingia kwenye mashamba ya wakulima kuharibu mazao.

Alisema wafugaji ni matajiri hivyo kutokana na maeneo ya kufugia kuwa changamoto kadri siku zinavyokwenda, imefika wakati wa wao kubadilika na kuanza kununua maeneo ambayo watakuwa huru kupanda nyasi za kutosha na kuchungia mifugo yao.

Ndaki alisema wakulima wana maeneo yao ambayo wanalima mazao mbalimbali hivyo umefika wakati wa wafugaji nao kununua maeneo ya kufugia ili wote watumie ardhi vizuri na iwanufaishe.

Aliwasisitiza kununua maeneo ya kufugia kulingana na mifugo waliyonayo ili wachunge kwa uhuru. Pia aliwataka wapande malisho badala ya kutegemea uoto wa asili pekee ambao hautoshi kulingana na mifugo kuwa mingi.

Pia aliwataka wafugaji kuanza kuvuna mifugo yao inapokuwa mingi ikiwa ni hatua ya kukabili uhaba wa maeneo ya kuchungia na ongezeko la watu na shughuli za kibinadamu.

Aliwasihi kuwekeza kwenye miradi mingine hasa hoteli, kutokana na fedha wanazopata baada ya kuuza mifugo yao.

"Binadamu tunazaliana, mifugo nayo inaongezeka, shughuli za kibinadamu zinaongezeka, mahitaji ya ardhi na matumizi yake yanaongezeka kwa kasi, lakini ardhi yetu haiongezeki iko palepale," alisema.

Mbunge wa Momba, alisema katika jimbo lake kumekuwa na changamoto ya muda mrefu ya migogoro kati ya wafugaji na wakulima kutokana na kuwapo wafugaji wengi na wakulima.

Alimuomba Waziri wa Mifugo na Uvuvi kuwaboreshea miundombinu ya usafiri ili kuboresha huduma za kuwafikia wafugaji ambao mifugo yao hufa kutokana na uhaba wa wataalamu na upungufu wa majosho.

Scanned with CamScanner